# SIRI YA UHAKIKA

**Na**

**Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian**

Masihi Mau'udi na Imam Mahdi
Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya
Tanzania

**SIRI YA UHAKIKA**
Raze Hakikat (Kiurdu)

Mwandishi:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

Mfasiri: Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya

© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): Qadian 1903
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): Tanzania 2016

Kwa maelezo zaidi:
Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dare es Salam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744
Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi, Kenya. Simu: +254222111031

Kimechapwa na: Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salam, Tanzania
Simu: +255222111031

ISBN: 978-1-84880-545-3

ٹائیٹل بار اول

# اے خدا اے چشمۂ نورِ ھُدیٰ
# از کرم ہا چشم این اُمت کشا
# یک نظر کن سوئے این رازِ نہان
# تا رہی اے طالب از وہم گمان

الحمد للہ والمنۃ

کہ یہ رسالہ جس کا نام ہے

# رازِ حقیقت

حضرت عیسیٰ علیہ السلام کے صحیح اور سچے سوانح ظاہر کرتا ہے اور ہمارے مباہلہ کے متعلق

کی نصیحتیں کرکے اصل غرض مباہلہ بتلاتا ہے

در مقام قادیان مطبع ضیاء الاسلام میں باہتمام حکیم فضل الدین صاحب
بھیروی مالک مطبع چھپا ہے اور بتاریخ
۳۰ر نومبر ۱۸۹۸ء
شایع ہوا

جلد ۲۱۰۰

Jalada la chapa ya kawanza

Ewe Mungu, ewe chemchemi ya nuru ya mwongozo,
kwa hisani yako ufumbue macho ya umati huu.
Uzingatie siri hii iliyofichikana,
ee mtafutaji, ili ujiokoe katika wasiwasi na shaka.

Sifa zote njema na hisani ni za Mwenyezi Mungu
kwabma kijitabu hiki kinachoitwa

# Siri ya Uhakika

kinabainisha habari sahihi na ya kweli ya maisha ya Hadhrat Isa a.s. na kwa kutoa nasaha kadhaa kuhusiana na mubahala wetu kinafafanua shabaha hasa ya mubahala.

Na kimechapwa katika kiwanda cha uchapaji 'Dhia-ul-Islam', chini ya usimamizi wa Bwana Hakim Fadhlud Din wa Bhera, mmliki wa kiwanda cha uchapaji, na kikaenezwa tarehe 30 Novemba 1898

Nakala: 2100

# MAELEZO YA MWENEZI

Seyidna Ahmad a.s., Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya aliandika kitabu '*Raze Hakikat*' ili kueleza matukio sahihi ya maisha ya Nabii Isa a.s. ambayo kwa watu wa kawaida yalikuwa ufichoni. Mikononi mwenu ndiyo tafsiri ya kitabu hicho kwa lugha ya Kiswahili kilichoitwa Siri ya Uhakika.

Ndani ya kitabu hiki shutuma za Sheikh Muhammad Husain wa Batala pia zimejibiwa vya kutosha.

Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya alikitafsiri kwa Kiswahili, kisha Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Amiri na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Tanzania kaisoma tafsiri kwa uangalifu akiilinganisha na matini ya Kiurdu. Kabla hakijapelekwa mtamboni nikaidurusu kikamilifu kwa makini.

Sheikh Ansar Hussain na Seyid Tanwir Mujtaba nao wakasaidia kwa njia mbalimbali ili kukamilisha kazi hii. Mungu Awape wote hao malipo bora hapa na huko akhera.

Jamil R. Rafiq
Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan.

6 Machi 2016

## Tangazo

Mkutano ulikuwa ukifanyika sikuzote katika likizo za Desemba. Lakini safari hii katika Desemba mimi na watu wa nyumbani mwangu na mahadimu wengi wanawake na wanaume wanaumwa kwa maradhi yatokanayo na majira. Kutakuwa na shida kuwahudumia wageni. Kuna sababu nyingine nyingi pia ambazo kuziandika hapa ni kurefusha tu maneno. Hivyo, inatangazwa kuwa safari hii mkutano hautafanyika. Ndugu zetu wote wawe na taarifa hii.

Wassalaam, Mtangazaji,

Mirza Ghulam Ahmad.

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ[1]

**نَحْمَدُہٗ وَنُصَلِّیْ عَلٰی رَسُوْلِہِ الْکَرِیْمِ** [2]

اِنَّ اللّٰہَ مَعَ الَّذِیۡنَ اتَّقَوۡا وَّ الَّذِیۡنَ ہُمۡ مُّحۡسِنُوۡنَ[3]

"مبادا دل آں فرد مایہ شاد

کہ از بہر دنیا دہد دیں بباد" [4]

Mimi ninatoa tangazo hili hasa kwa ajili ya Jumuiya yangu kuwa wasubiri matokeo ya tangazo lile lililotangazwa tarehe 21 Novemba 1898 kuhusiana na mubahala wa Sheikh Muhammad Husain wa Batala, mhariri wa Isha'at Sunna na marafiki zake wawili, ambao muda wake utaishia tarehe 15 Januari 1900.

Nami nasema maneno machache ya nasaha kwa Jumuiya yangu kuwa wakishikamana na ucha Mungu

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. Mwenezi

[2] Tunamhimidia Yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu. Mwenezi

[3] Kwa hakika Allah Yu pamoja na wale wanaomcha, na wale wafanyao wema. An-Nahl, 16:129. Mwenezi

[4] Moyo wa huyu mdhalili usipate raha ambaye ameharibu dini kwa ajili ya dunia. Mwenezi

wasipayuke kushindana na wapayukao, na wasishindane katika kutoa matusi. Wao watasikia kebehi na dhihaka nyingi kama wanavyozisikia hivi sasa. Lakini wanatakiwa wakae kimya na wausubiri uamuzi wa Mwenyezi Mungu wakimcha Mungu, wakiwa na bahati njema. Wakitaka wawe wenye kusaidiwa machoni mwa Mwenyezi Mungu, basi wasiachane na wema, subira na ucha Mungu. Sasa faili la kesi liko mbele ya mahakama ile isiyompendelea yeyote, na isiyopenda njia za ujeuri. Pale mtu anapokuwa nje ya chumba cha mahakama, ingawa hushikwa pia kwa sababu ya maovu yake, lakini adhabu ya yule mtu huwa kali sana ambaye akisimama mahakamani anafanya uhalifu kwa ujeuri. Hivyo, nawaambieni mwogope kudharau Mahakama ya Mwenyezi Mungu, na shikeni upole, unyenyekevu, subira na ucha Mungu, na muombeni Mwenyezi Mungu kuwa Atoe uamuzi baina yenu na kaumu yenu. Afadhali msikutane kabisa na Sheikh Muhammad Husain na marafiki zake, kwani wakati mwingine kukutana kwasababisha mapigano na mabishano. Na ni vyema katika kipindi hiki msifanye nao majadiliano, kwani wakati mwingine majadiliano husababisha maneno makali. Ni lazima mpige hatua katika kutenda mema, unyoofu na ucha Mungu, maana Mungu kamwe Hawatupi wale wanaoshikamana na ucha Mungu. Hebu angalieni,

Nabii Musa a.s aliyekuwa mpole na mcha Mungu kuliko wote katika zama zake alipataje ushindi dhidi ya Firauni kwa baraka za ucha Mungu. Firauni akataka kumwangamiza yeye, lakini Mwenyezi Mungu Akamwangamiza Firauni pamoja na majeshi yake yote mbele ya macho ya Hadhrat Musa a.s. Tena katika zama za Hadhrat Isa a.s. Mayahudi wenye bahati mbaya wakapenda wamwue, na siyo kumwua tu, bali na kutia doa la laana katika roho yake takatifu kwa kumwua msalabani. Kwani iliandikwa ndani ya Torati kwamba mtu anayekufa juu ya mti, yaani msalabani, huyo amelaaniwa, yaani moyo wake huwa mchafu na najisi naye hutupwa mbali na ukaribu wa Mungu, na hukataliwa katika baraza la Mungu na huwa kama shetani; ndiyo maana jina la shetani ni "Laiin" (mlaaniwa). Huo ulikuwa mpango mbaya sana uliopangwa dhidi ya Hadhrat Masih a.s. ili kaumu hiyo mbovu imchukulie mtu huyo kuwa si mwenye moyo uliotakasika wala si nabii mkweli wala siye mpendwa wa Allah, kwani, Mungu Apishe mbali, yu mlaaniwa ambaye moyo wake haukutakasika, na — kama ilivyo maana ya laana — yeye amchukia Mungu na Mungu Amchukia yeye. Lakini Mungu Mweza na Mhifadhi wa milele Aliwafanya Mayahudi wenye nia mbaya washindwe kutimiza nia yao na wasipate lengo lao. Na siyo tu kwamba Mungu Akamwokoa nabii wake mtakatifu katika kifo cha

msalabani, bali Akimbakiza hai hadi miaka mia moja na ishirini,[5] na Akawaangamiza maadui zake wote wa Kiyahudi mbele ya macho yake. Naam, sawa na suna

---

[5] Kutokana na Hadithi sahihi inathibitika kuwa Hadhrat Isa a.s. alipata umri wa miaka mia moja na ishirini. Lakini kwa makubaliano ya Wayahudi na Wakristo wote, tukio la msalaba lilitokea wakati ambapo umri wake ulikuwa miaka thelathini na mitatu tu. Dalili hii inaonyesha kuwa Nabii Isa a.s., kwa fadhili za Allah, akinusurika na kifo cha msalabani akapitisha umri uliobakia katika kutalii. Kutokana na hadithi sahihi, inathibitika pia kwamba Hadhrat Isa a.s. alikuwa Nabii mtalii. Hivyo, kama baada ya tukio la msalaba yeye alipaa mbinguni na mwili wake, basi akatalii zama gani ilhali wataalamu wa lugha pia wanaeleza sababu moja ya neno Masihi ni kuwa hilo limetokana na neno *mas-h*, na *mas-h* maana yake ni kutalii. Isitoshe, itikadi hii kuwa ili kumnusuru Hadhrat Isa na Mayahudi, Mungu Akampandisha kwenye mbingu ya pili, yaonekana ni wazo la kipuuzi kabisa, kwani kwa kitendo hiki cha Mungu hoja haikamiliki juu ya Mayahudi. Mayahudi hawakumwona akipaa mbinguni wala mpaka leo hawajamwona akishuka, basi wanawezaje kukiamini kisa hiki kisicho na maana, kisichokuwa na uthibitisho? Mbali na hili yapasa kufikiria kuwa Mwenyezi Mungu Alimsalimisha Mtume wake Seyyidna Muhammad s.a.w. wakati wa mashambulio ya Makuraishi waliokuwa mashujaa zaidi na wapiganaji vita na wenye kinyongo zaidi kuliko Mayahudi, Akimlinda ndani ya pango lile lisilokuwa mbali zaidi ya maili tatu kutoka mji mtukufu wa Makka.

ya zamani ya Mwenyezi Mungu – kwamba hakuna nabii yeyote mwenye imara aliyepita ambaye

---

Je, Mungu Apishe mbali, Mwenyezi Mungu Aliwahofia Mayahudi waoga kiasi hiki kwamba pasipo kumpeleka kwenye mbingu ya pili hakuweza kutulia kwa hofu ya ujeuri wa Mayahudi. Bali kisa hiki ni cha kubuniwa tu, nacho ni kinyume na Kurani Tukufu, na kinathibitika kuwa cha uongo kwa hoja madhubuti. Tumeshaeleza kwamba kwa kukagua ukweli wa tukio la msalaba, Marhamu ya Isa ni njia moja ya kielimu na ni kipimo cha hali ya juu cha kuutambua ukweli. Nami nalifahamu tukio lote hili vizuri kwa kuwa mimi ni mtu ninayetokana na ukoo wenye ujuzi wa utabibu. Baba yangu, Marehemu Mirza Ghulam Murtadhaa aliyekuwa mtemi wa kuheshimika katika wilaya hii, alikuwa pia tabibu mkubwa wa ngazi ya juu sana ambaye alitumia miaka sitini ya umri wake akifanya mazoezi makubwa na kadiri ilivyowezekana alikusanya vitabu vingi sana vya utabibu. Nami mwenyewe nimevisoma vitabu vya utabibu na daima nilivipitia. Hivyo basi mimi kutokana na ujuzi wangu binafsi ninaeleza kuwa vitakuwa vitabu zaidi ya elfu moja ambamo mmeandikwa habari za marhamu ya Isa, na imeandikwa pia humo kuwa marhamu hii ilitengenezwa kwa ajili ya Hadhrat Isa a.s. Miongoni mwa vitabu hivyo, vipo vitabu vya Wayahudi na vingine ni vya Wakristo na vingine ni vya Mamajusi. Hivyo, ushahidi huu unapatikana baada ya kufanya utafiti wa kielimu kuwa Nabii Isa a.s. lazima alisalimika kutoka msalabani. Kama waandishi wa Injili wameandika kinyume chake, basi ushahidi wao haufai kuaminika hata chembe, kwani,

hakuhama kutokana na mateso ya kaumu yake – Hadhrat Isa a.s. pia baada ya kuhubiri kwa miaka

---

kwanza kwa vile hao hawakuwepo wakati wa tukio la msalaba, na wote wakamkimbia Bwana wao wakimsaliti. Pili ni kwamba ndani ya Injili kuna hitilafu nyingi sana, hata kwamba ndani ya Injili ya Barnabas imekataliwa Hadhrat Masihi kufia msalabani. Tatu ni kwamba ndani ya Injili hizo hizo zinazofikiriwa kuaminika sana imeandikwa kuwa baada ya tukio la msalaba Hadhrat Masihi a.s. alikutana na wanafunzi wake na akawaonyesha majeraha yake. Basi, kutokana na taarifa hii, yaonekana wakati huo majeraha yalikuwepo yaliyohitaji marhamu itayarishwe. Hivyo, yaeleweka kwa yakini kabisa kuwa marhamu ile ilitayarishwa wakati huo. Na inathibitika kutokana na ma-Injili kuwa Hadhrat Isa a.s. alikaa katika maeneo hayo akijificha kwa muda wa siku arobaini, na alipopata kupona kabisa kutokana na matumizi ya marhamu hiyo ndipo akawa anasafiri. Inasikitisha kuwa Daktari mmoja ametoa kipeperushi kutoka Rawalpindi ambamo amekataa kuwa marhamu ya Isa haikupata kuandikwa ndani ya vitabu vya mataifa mbalimbali. Yaonekana akafadhaika na kufikiria kuwa muradi wote wa kafara hubatilika kwa kusikia Hadhrat Isa a.s. hakufia msalabani bali akaokolewa akiwa hai, lakini alikuwa majeruhi, Lakini ni jambo la aibu sana kukanusha kuwepo kwa vitabu vile ambamo imeandikwa dawa hii ya marhamu ya Isa. Kama yu mtafuta haki, basi na aje huku kwetu akavione vitabu hivyo. Na sio huu tu msiba kwa ajili ya Wakristo kuwa ushahidi wa kielimu wa marhamu ya Isa unazipinga itikadi hizo

mitatu akahamia upande wa India akisalimika na jaribio la fitina ya msalaba. Kisha akayafikishia

---

na papo hapo jengo lote la kafara na utatu linaporomoka, bali siku hizi thibitisho zingine zimepatikana zinazoutilia nguvu ushahidi huu. Kwani utafiti unathibitisha kuwa hakuna budi Hadhrat Masihi a.s. baada ya kunusurika katika tukio la msalaba akasafiri kwenda India akipitia Nepal, hatimaye akafika Tibat, kisha akaishi Kashmir kwa muda fulani na wale wana wa Israeli waliokuja kuishi Kashmir baada ya kutokea vurugu huko Babil akawaongoza. Hatimaye akafariki dunia mjini Srinagar akiwa na umri wa miaka mia moja na ishirini na akazikwa katika mtaa wa Khanyar. Na kutokana na mabadiliko ya kimatamshi ya wenyeji wa huko akawa maarufu kwa jina la Nabii Yuz Asaf.* Habari hii hata Injili inasadikisha iliyogunduliwa

---

*Tanbihi: Mwislamu mmoja asiye na ujuzi akifikiria moyoni mwake akasema huenda Yuz Asaf muradi wake ni mke wa Asaf aliyekuwa waziri wa Suleiman. Lakini jahili huyo hakufikiria kuwa mkewe Asaf hakuwa Nabii wala hawezi kuitwa mwanamfalme. Hakuyafikiria majina yote haya kuwa ni ya kiume. Hata kama angekuwa na sifa hizo, basi angeitwa nabiyyah (nabii wa kike) na binti mfalme, siyo nabii wala mwanamfalme. Mtu huyo mwenye ujuzi haba hata hakuzingatia kuwa muda wa miaka elfu moja na mia tisa unaafikiana tu na zama za Hadhrat Isa a.s. Suleiman alikuwepo miaka mia kadhaa kabla ya Nabii Isa a.s. Mbali na hayo, kaburi la nabii huyo lililopo Srinagar, baadhi ya watu huliita kaburi la Yuz Asaf, lakini watu wengi wanasema kuwa kaburi hili ni la nabii Isa a.s. Ndugu yetu mwaminifu Maulawii Abdullah Mkashmiri alipoanza kufanya utafiti kuhusiana na kaburi hili, baadhi ya watu waliposikia jina la Yuz Asaf wakasema kuwa kwetu sisi kaburi hili linajulikana kuwa

ujumbe mataifa mengine ya Wayahudi walioenea India, Kashmir na Tibet baada ya mfarakano wa

---

hivi karibuni huko Tibat. Injili hii ilipatikana kwa taabu sana huko London. Rafiki yetu mwaminifu, Bwana Sheikh Rahmatullah, mfanyabiashara, alikaa huko London karibu miezi mitatu akiitafuta Injili hiyo. Mwishowe ilipatikana katika sehemu fulani. Injili hii ni kama sehemu ya kitabu cha zamani cha dini ya Kibudha. Ushahidi unapatikana ndani ya vitabu vya Kibudha kuwa Hadhrat Isa a.s. alikuja nchini India, na kwa muda fulani aliendelea kuwapa mawaidha watu wa mataifa mbalimbali. Na katika vitabu vya Kibudha mlimoelezwa kufika kwake katika nchi hii, sababu yake siyo ile iliyoelezwa na kina Lama (watawa wa Kibudha) kwamba Yeye (Nabii Isa) alipata mafundisho ya Gautama Budha. Kusema hivyo ni ukorofi, bali ukweli wenyewe ni huu kuwa Mwenyezi Mungu Alipomwokoa Hadhrat Isa a.s. katika tukio la msalaba, hapo hakuona masilahi kuendelea kuishi katika nchi hiyo. Na kama vile Mtume s.a.w. wakati wa dhulma kubwa ya Makuraishi yaani pale waliponuia kumwua Mtume s.a.w., alivyohama nchi yake, ndivyo Hadhrat Isa a.s. alivyohama wakati wa kilele cha ukatili wa Mayahudi, yaani wakati walipopanga njama za kumwua. Na kwa vile katika tukio la Bukhta Nassar (Nebuchadnezar), wana wa Israeli wakitawanyika wakaelekea nchi za India, Kashmir, Tibet na China, hivyo Hadhrat Masihi a.s. akaona hakuna budi ahamie nchi hizo. Na kutokana na historia yajulikana pia kwamba baadhi ya Mayahudi walifika

---

ni la Bwana Isa. Ilmuradi, watu wengi wanaoishi Srinagar mpaka leo wanatoa ushahidi huu. Yeyote anayeshuku aende mwenyewe Kashmir akawaulize malaki ya watu kule. Sasa baada ya hayo kukataa ndio ukosefu wa haya. Mwandishi

Babil. Hatimaye akafariki dunia katika ardhi ya Kashmir iliyo mfano wa Pepo, na akazikwa katika

---

nchi hiyo na kwa sababu ya mazoea yao ya zamani wakajiunga pia na dini ya Kibudha. Hivi karibuni makala moja imechapishwa ndani ya gazeti la kila siku la "The Civil & Military Gazette" la tarehe 23 Novemba 1898, ambamo mhakiki mmoja Mwingereza amekiri na kukubali jambo hili kuwa baadhi ya makundi ya Mayahudi walifika katika nchi hiyo na kuishi nchini humo. Na katika toleo hilo hilo la "Civil" imeandikwa kuwa "kwa kweli Maafghani pia ndio miongoni mwa Wana wa Israeli." Ilmuradi, Wana wa Israeli walipoingia ndani ya dini ya Kibudha, basi ilibidi Hadhrat Isa a.s. akiwasili nchi hiyo aelekee kukanusha dini ya Kibudha na akutane na viongozi wa dini hii, na ndivyo ilivyokuwa. Ndiyo maana maisha ya Hadhrat Isa a.s. yakaandikwa ndani ya vitabu vya dini ya Kibudha. Inaonekana kuwa wakati huo dini ya Kibudha ilikuwa na nguvu sana nchini humo na dini ya Veda ilikuwa imekufa na dini ya Kibudha ilikuwa imeikataa Veda.*

Kwa kifupi ni kuwa kwa kuyajumuisha mambo hayo yote, matokeo ya lazima ni kwamba hakuna budi Hadhrat Isa a.s. alikuja tu nchini humo. Hili ni jambo la yakini na imara kuwa ndani ya vitabu vya Kibudha mmeelezwa kuja kwake nchini humo. Na kaburi la Hadhrat Isa a.s. lililopo Kashmir linaloongelewa kuwa lipo hapo tangu karibu miaka 1900, ni ushahidi wa hali ya juu kabisa juu ya jambo hili. Huenda pamoja na kaburi hilo yapo

---

*Si hili tu kwamba katika baadhi ya vitabu vya dini ya Kibudha mmeelezwa kuwa Hadhrat Masihi a.s. alikuja India na Tibeti, bali tumejua kwa njia za kutegemewa kwamba jambo hili lemeelezwa katika maandiko ya zamani ya Kashmir pia. — Mwandishi

mtaa wa Khanyar kwa heshima zote. Kaburi lake lajulikana sana, latembelewa na kuchukuliwa baraka

---

maandiko ambayo hivi sasa yamefichikana. Kwa ajili ya kufanya utafiti zaidi wa mambo haya, kafila kwa uchunguzi wa kielimu inaandaliwa katika Jumuiya yetu itakayoongozwa na ndugu yangu Maulawii Hakiim Alhaji Bwana Nuruddin, Mola wake amlinde. Kafila hiyo itatembelea nchi mbalimbali kufanya utafiti na uchunguzi huo. Waaminio hao watakuwa na wajibu kuviangalia pia vitabu vya lugha ya Kipali, kwani imepatikana pia habari kuwa Hadhrat Masihi a.s. aliendа maeneo hayo vile vile akiwatafuta kondoo zake waliopotea. Lakini kwa vyovyote kwenda Kashmir, kisha Tibeti, ili kutafuta hayo yote kutoka ndani ya vitabu vya dini ya Kibudha, litakuwa ni jukumu la jamaa hao. Ndugu yangu Bwana Sheikh Rahmatullah, mfanyabiashara wa Lahore, amejichukulia jukumu la kutoa gharama zote hizi. Lakini safari hii, kama inavyofikiriwa, ifanywe mpaka Banaras, Nepal, Madras, Swat, Kashmir, Tibeti na nchi nyinginezo — popote pale pajulikanapo akaishi Hadhrat Masihi a.s. Basi, bila shaka kazi hii inahitaji gharama kubwa na inatarajiwa kwa hali yoyote ile kwamba Mwenyezi Mungu Ataikamilisha. Kila mtu mwenye busara anaweza kuelewa kuwa huu ni uthibitisho unaouvunjilia mbali mara moja mfumo wa dini ya Kikristo, na mpango wote wa tangu miaka 1900 unafutika papo kwa papo. Jambo hili limeturidhisha kwamba ujaji wa Hadhrat Masihi a.s. nchini India na Kashmir n.k. ni jambo la kweli, na kuhusiana na habari hii shuhuda madhubuti zimepatikana zisizoweza kufichikana kwa hila ya mpinzani yeyote. Inaonekana kwamba itikadi hizo potofu na za uwongo zilikuwa zidumu tu hadi zama hizi. Kauli hii ya Seyidna na Maulana, mbora wamanabii s.a.w. kuwa Masihi Mau'udi anayetegemewa kuja atavunja msalaba na kwa silaha za kimbingu

kwalo.

Vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu kwa usaidizi wa aina

---

atamwua dajali, muradi wa Hadithi hii umejulikana sasa kuwa katika zama za Masihi huyo, Mungu wa mbingu na ardhi Ataleta kutoka Kwake baadhi ya mambo na matukio ambayo kwayo itikadi za msalaba, utatu na kafara zitajifia zenyewe. Kushuka kwa Masihi kutoka mbinguni pia kwamaanisha kuwa wakati huo, kwa dhamira ya Mungu wa mbingu zitapatikana shuhuda za wazi kabisa za kuuvunja msalaba. Na ndivyo ilivyotokea. Ni nani aliyejua kuwa dawa ya marhamu ya Isa itakuja kutwa kuandikwa ndani ya mamia ya vitabu vya utibabu? Nani alikuwa na habari hii kwamba kutoka ndani ya vitabu vya zamani vya Kibudha ushahidi utapatikana kuwa Hadhrat Isa a.s. baada ya kukata tamaa na Mayahudi wa nchi ya Sham, alielekea India, Kashmir na Tibeti.* Nani alijua kuwa kaburi la Hadhrat Isa a.s. liko Kashmir? Je, mwanadamu angeweza kwa nguvu yake kudhihirisha mambo hayo? Sasa matukio hayo yanaufuta Ukristo kama vile usiku unavyofutika kunapokucha. Kuthibitika kwa tukio hili, dini ya Kikristo inapata pigo linaloweza kulipata paa ambalo uzito wake wote ulikuwa juu ya boriti moja; boriti likavunjika na paa likaanguka. Ndivyo hivyo ifikiavyo mwisho dini ya Kikristo

---

*Siku hizi vimepatikana vitabu vichache vya zamani vilivyoandikwa na Waislamu pia ambamo imeandikwa waziwazi kuwa Yuz Asaf alikuwa mtume, aliyetoka nchi fulani naye alikuwa mwanamfalme na akafia Kashmir. Na imeelezwa kuwa nabii huyo alipita miaka 600 kabla ya Mtume wetu Muhammad s.a.w. — Mwandishi.

aina Akamfaulisha Sayidna na Maulana Nabii wa

---

kwa kuthibitika tukio hili. Mungu Hufanya Anayoyataka. Kwa kudra kama hizo Amejulikana. Hebu angalieni maana nzuri ilioje iliyothibitika ya aya hii:

وَمَا قَتَلُوهُ وَمَا صَلَبُوهُ وَلٰكِنْ شُبِّهَ لَهُمْ *

Yaani kumwua na kumfisha Masihi msalabani, yote ni uongo mtupu. Ukweli wenyewe ndio huu kuwa watu hao walidanganyika, na Masihi a.s., sawa na ahadi ya Mungu akisalimika msalabani akaenda. Na kama Injili ikisomwa kwa uangalifu, basi Injili nayo inatoa ushahidi uo huo. Je dua ya Masihi aliyoyaomba usiku kucha kwa unyenyekevu ingeweza kukataliwa? Je, kauli ya Masihi kwamba nitakaa kaburini kwa siku tatu kama Yunus yaweza kumaanisha kuwa alikaa kaburini akiwa mfu? Je, Yunus alikaa tumboni mwa samaki kwa siku tatu akiwa mfu? Je ndoto ya mkewe Pilato haionyeshi utashi huu wa Mungu kwamba Atamuokoa msalabani? Kadhalika, Masihi kutundikwa msalabani saa za mwisho katika siku ya Ijumaa na kuteremshwa kabla ya jioni na kutobakia msalabani kwa siku tatu sambamba na desturi za kale na kutovunjiwa mifupa, na kutokwa na damu, je mambo hayo yote hayanadi kwa sauti ya juu kuwa sababu zote hizo zimeandaliwa tu kwa kumwokoa Masihi? Na kwa kuomba tu dua, sababu hizo za rehema zikadhihiri. Yaliwezaje kukataliwa maombi ya mtu aliye mpendwa wa Mungu yaliyoombwa usiku kucha kwa vilio? Kisha Masihi kuonana na wanafunzi wake na kuonyesha majeraha baada ya kuondolewa msalabani ni dalili madhubuti ilioje juu ya kutokufa kwake msalabani. Na kama sivyo, basi sasa mwiteni Masihi aje kukutana nanyi kama alivyokutana na wanafunzi. Ilmuradi, inathibitika kwa kila jiha kwamba Hadhrat Masihi a.s. alisalimika

---

*An-Nisaa, 4:158. Mwenezi

zama za mwisho aliyekuwa Mkuu wa watawa. Ingawa mwanzoni yeye pia, kama Hadhrat Musa a.s. na Hadhrat Isa a.s., alipata shida ya kuhama, lakini

---

msalabani na akaja katika nchi hii ya India, kwa sababu makundi kumi ya Wana wa Israeli yalikuja katika nchi hizi ambao mwishoni wakawa Waislamu. Na baada ya kusilimu, kwa mujibu wa ahadi ya Torati, wakapatikana miongoni mwao wafalme wengi pia. Na hii ni dalili moja ya ukweli wa unabii wa Mtume s.a.w., maana ndani ya Torati kulikuwa na ahadi kwamba Wana wa Israili wakimfuata Nabii aliyeahidiwa watapata utawala na ufalme. Hivyo basi, kumwua Masihi mwana wa Mariamu msalabani ni chanzo ambacho msingi wa kanuni zote za dini kama vile kafara na utatu na kadhalika umewekwa juu yake. Na hili ndilo wazo lililopenya katika mioyo ya Wakristo milioni mia nne na kwa kuuthibitisha ubatili wake, dini ya Kikristo haibaki chochote wala lolote. Kama katika Wakristo kuna kundi lolote lenye jadhba ya utafiti wa kidini, basi yumkini baada ya kupata habari ya thibitisho hizo waiage haraka sana dini ya Kikristo. Na kama moto wa utafiti huu ulipuke mioyoni mwa watu wote wa Ulaya, basi lile kundi la watu milioni mia nne lililojiandalia kwa miaka elfu moja na mia tisa, yawezekana kwa msaada wa Mungu ndani ya miezi kumi na tisa ligeuke na kusilimu, kwani baada ya itikadi ya kimsalaba kuthibitika kuwa Hadhrat Masihi a.s. hakufia msalabani bali kaendelea kutembelea nchi zingine ni jambo ambalo latowesha mioyoni itikadi za Kikristo mara moja na kuleta mapinduzi makubwa katika ulimwengu wa Ukristo.

Enyi wapendwa! Sasa iacheni dini ya Kikristo, maana Mungu Ameshaonyesha ukweli. Njooni kwenye mwanga wa Islam mkapate wokovu. Na Mungu Mjuzi Anajua ya kuwa nasaha yote hii imetolewa kwa nia njema na baada ya kufanya utafiti mkamilifu. Mwandishi.

uhamaji huo ulikuwa na vyanzo vya ushindi na nusura ndani yake. Hivyo basi, enyi marafiki! eleweni kwa yakini kuwa mcha Mungu haangamizwi kamwe. Makundi mawili yanapokuwa maadui na kufikisha uhasama hadi mwisho, basi lile kundi ambalo machoni mwa Mwenyezi Mungu ni lenye utawa na wema ndilo huteremkiwa msaada kutoka mbinguni, na kwa njia hii mizozo ya kidini hupata kuamuliwa kwa maamuzi ya kimbinguni. Hebu angalieni, katika hali ya unyonge kiasi gani Sayidna na Maulana Nabii wetu Hadhrat Muhammad s.a.w. alidhihiri mjini Maka, na siku hizo Abu Jahli na wengineo walikuwa na uluwa mkubwa namna gani. Malaki ya watu wakawa maadui wenye hamu ya kumwua Mtume s.a.w. Basi kilikuwa ni kitu gani kilichomfaulisha Nabii wetu Mtukufu s.a.w. na kumshindisha? Eleweni kwa yakini kuwa huu ndio ulikuwa uongofu, uaminifu, utakaso na ukweli. Hivyo basi, enyi ndugu! Fuateni nyayo hizi, na ingieni ndani ya nyumba hii kwa nguvu sana, kisha hivi karibuni mtaona kuwa Mwenyezi Mungu Anawasaidieni. Mungu Yule Anayefichikana machoni, lakini ndiye Ang'aaye zaidi kuliko vitu vyote Ambaye hata malaika pia wanamwogopa kwa jalali yake, Yeye hapendi ukosefu wa adabu na ujanja, na huwahurumia wanaomwogopa. Hivyo, Mwogopeni na neneni kila neno baada ya kulizingatia. Nyinyi ni watu wa

Jumuiya yake Aliowachagueni ili mwonyeshe mfano wa wema. Basi, yule asiyeacha uovu, na midomo yake haiepuki uongo na moyo wake hautengani na mawazo machafu, mtu huyo atatengwa na Jumuiya hii. Enyi watu wa Mungu! isafisheni mioyo na jitakaseni undani mwenu. Mwaweza kumridhisha kila mmoja kwa unafiki na udumakuwili wenu, lakini kwa tabia hii mtamghadhabisha Mungu. Jihurumieni nafsi zenu na viepusheni vizazi vyenu na maangamio. Haiwezekani kamwe Mungu Awaridhie ilhali mioyoni mwenu kuna mwingine mnayempenda zaidi kuliko Yeye. Jitoleeni katika njia yake na jishughulisheni kwake hata kusahau mengine na kuweni wake kikamilifu, kama mkitaka kumwona Mungu katika dunia hii hii. Mwujiza ni nini na mambo ya ajabu hutokea lini? Hivyo eleweni na kumbukeni kuwa mabadiliko ya kiroho yanahitaji mabadiliko ya mbingu. Moto ule unaowaka kwa ikhlasi, huo huuonyesha ulimwengu wa juu kwa sura ya ishara fulani. Waaminio wote, ingawa kwa kawaida hushiriki katika kila jambo hata kwamba kila mmoja hupata ndoto za kawaida na baadhi yao hupata ufunuo pia, lakini mwujiza wenye jalali ya Mungu na mng'ao ndani yake na ambao wamwonyesha Mungu, huo huwa ni nusura maalum ya Mungu inayodhihirishwa kuwazidishia heshima watu ambao wana daraja la kujitoa kwa Mungu aliye Mmoja, ilhali

wanadhalilishwa duniani nao wanaitwa kuwa wabaya, na wanaitwa waongo, wazushi, na waovu, walaaniwa, madajjali, wadanganyifu na walaghai na juhudi zafanywa kuwaangamiza, lakini hufanya subira kwa muda na kujizuia, kisha ghera ya Mwenyezi Mungu hutaka kuonyesha ishara kwa kuwasaidia. Ndipo, mara moyo wao huudhika na kifua chao kujeruhika, basi wao hukiangukia kizingiti cha Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu, na dua zao zenye uchungu husababisha kelele za vilio huko mbinguni. Na kama vile, baada ya joto kali, viwingu vidogo vidogo hudhihirika mbinguni, kisha kwa kuunganika pamoja kwa kupangana juu kwa juu kukawa wingu la mvua na mara mvua huanza kunyesha, vivyo hivyo vilio vya uchungu vya waaminifu ambavyo vinakuwa katika wakati wake vinavyoinua mawingu ya rehema na hatimaye kwa sura ya ishara huteremka ardhini. Ilmuradi, pale mtu mkweli, walii wa Allah, anapofanyiwa dhuluma kupindukia, hapo yafaa ieleweke kuwa sasa ishara itadhihirika.

ہر بلا کیں قوم را حق دادہ است
زیر آں گنج کرم بنہادہ است[6]

Hapa ninalazimika kuandika kwa masikitiko kuwa

---

[6] Balaa lolote Mungu Analowapatia watu hawa, huwa Anaweka rehema chini yake. Mwenezi

wapinzani wetu hawajiepushi na utovu wa uadilifu, uongo, na ukaidi. Wanajasiri kuyakadhibisha maneno ya Mungu na huzikataa ishara za Mungu Mwenye jalali. Nilitumai kuwa baada ya kipeperushi changu cha tarehe 21 Novemba 1898, kilichoandikwa dhidi ya Sheikh Muhammad Husain wa Batala na Muhammad Bakhsh Ja'far Zatalli na Abul Hasan Mtibeti, watu hawa watanyamaza, kwani ndani ya kipeperushi mlikuwa na maneno ya wazi kuwa muda hadi 15 Januari 1900 umekwishawekwa kwa jambo hili kwamba yule mtu atakayekuwa mwongo, Mungu Atamdhalilisha na kumfedhehesha. Na hiki ndicho kilikuwa kipimo cha wazi kabisa kwa kumpambanua mkweli na mwongo alichokiweka Mwenyezi Mungu kwa ufunuo wake. Iliwapasa watu hawa kukaa kimya na kusubiri uamuzi wa Mungu mpaka tarehe 15 Januari 1900. Lakini yasikitisha kuwa hawakufanya hivyo, bali huyo Zatalli akajaza tena uchafu katika kipeperuchi chake cha tarehe 30 Novemba 1898 kama ilivyo tabia yake sikuzote na akaongopa moja kwa moja. Katika kipeperushi hicho anaandika kuwa hakuna bishara yoyote ya mtu huyo — yaani mimi — iliyotimia. Nisemaje kumjibu isipokuwa kwamba 'Laana ya Mungu iwe juu ya waongopao. Yuasema pia kuwa bishara inayomhusu Atham haikutimia. Kwa kujibu hatuwezi kusema chochote tena ila 'Laana ya Mungu iwe juu ya waongopao.' Ukweli wenyewe ni

kuwa moyo wa mtu unapokuwa mweusi kutokana na ubahili na inadi, mtu huyo huwa haoni japo anaona, na hasikii hali anasikia. Muhuri wa Mungu hugongwa juu ya moyo wake. Masikioni mwake mwatiliwa vizibio. Nani amefichikiwa hadi sasa jambo hili kwamba bishara iliyomhusu Atham ilikuwa na masharti, na ufunuo wa Allah ulidhihirisha kuwa katika hali ya kuelekea kwenye haki ndani ya muda uliowekwa, yeye atasalimika na kifo. Na kisha Atham akathibitisha kwa amali yake na kauli yake, kwa wasiwasi wake na hofu yake, na kwa kutokula kiapo na kutoshtaki kwake, kuwa ndani ya kipindi cha bishara moyo wake haukubaki imara juu ya Ukristo, na adhama ya Islam ikaingia moyoni mwake. Na hili halikuwa jambo lisilowezekana, kwani yeye alikuwa mtoto wa Waislamu, lakini aliritadi kutokana na baadhi ya sababu fulani. Yeye alikuwa na uelekeo fulani wa Kiislamu, ndiyo maana hakuiafiki itikadi ya Wakristo kikamilifu, na tangu awali alikuwa na dhana njema juu yangu. Hivyo, yeye kuiogopa bishara ya Kiislamu ni jambo linalowezekana. Kisha asipokula kiapo kwa kuuthibitisha Ukristo wake, wala hakunishtaki, bali akawa anaogopaogopa tu kama mwizi, na hata kwa juhudi kubwa za Wakristo pia hakuwa tayari kufanya hayo mambo, je, vitendo vyake hivyo si vyenye kuhakikisha kwamba lazima alikuwa anaiogopa adhama ya bishara ya Kiislamu. Watu

wenye maisha ya kughafilika huyaogopa hata matabiri ya wanajimu, sembuse bishara iliyotolewa kwa nguvu sana ambayo alipoisikia tu papo hapo rangi yake ikawa imefifia, ambayo pamoja nayo niliahidi kukubali kuadhibiwa isipotimia hiyo bishara. Basi, kwa nini hofu yake isingeingia ndani ya mioyo iliyonyimwa ukweli! Tena, kwa kuwa jambo hili halikubakia kuwa la kukisia tu, bali Atham mwenyewe aliidhihirisha fadhaa yake ya ndani na mabadiliko ya hali yake ya kiitikadi kutokana na hofu yake, mashaka yake na kutishika ambavyo vyote hivyo vilishuhudiwa na mamia ya watu. Na kisha baada ya kupita muda akaifikisha hali hiyo ya mabadiliko kwenye upeo wa yakini kwa kutokula kiapo na kutokunishtaki, kisha sawa na ufunuo wa Mwenyezi Mungu, akafa ndani ya miezi sita kutokea tangazo langu la mwisho. Je, matukio hayo yote hayajazi yakini moyoni mwa mwadilifu na mcha Mungu kwamba yeye aliendelea kuishi katika muda wa utabiri kwa kujinufaisha na sharti lililowekwa ndani ya ufunuo wa Mungu, kisha akafariki sawa na taarifa ya ufunuo wa Mwenyezi Mungu kwa kuuficha ushahidi. Sasa angalieni, tafuteni kuwa Atham yuko wapi. Je yuko hai? Je sio kweli kuwa yeye ameishakufa miaka mingi iliyopita? Lakini yule mtu ambaye huyo Atham alishindana naye katika jumba la Dkt. Clark huko Amritsar, yu hai mpaka sasa ambaye saa hizi

anaandika makala hii. Enyi msioona haya, hebu lifikirieni kidogo jambo hili kuwa kwa nini baada ya kuuficha ushahidi akafa upesi? Katika uhai wake mimi niliishaandika pia kuwa kama mimi ni mwongo, nitakufa kwanza, waila nitashuhudia kifo cha Atham. Basi kama mna haya, mtafuteni Atham yuko wapi? Yeye alikuwa anakaribiana nami katika umri na alikuwa anafahamiana na mimi kwa miaka thelathini. Kama Mungu Angetaka, Atham angeweza kuishi miaka mingine thelathini. Basi ilikuwaje yeye katika siku hizo hizo akafa kwa muafaka wa ufunuo wa Mungu ambapo kwa ajili ya kuwaliwaza Wakristo akauficha ukweli wa utabiri wa kiufunuo na kurejea kwa moyo wake kwenye haki. Mungu Anailaani mioyo inayoukataa ukweli baada ya kuukuta. Na kwa vile kukataa huku kulikofanywa na Wakristo na baadhi ya Waislamu wenye shari kulikuwa dhuluma ya wazi katika macho ya Mwenyezi Mungu, kwa hiyo kwa ajili ya kuitimiza bishara nyingine kubwa, yaani kwa bishara kuhusu kifo cha Pandit Lekhram, Akawadhalilisha na kuwafedhehesha kabisa wakataaji. Bishara hii ilikuwa ya ajabu kiasi hiki kwamba ndani yake ilielezwa mapema, yaani miaka mitano kabla, kuwa Lekhram atakufa siku gani na kifo cha aina gani. Lakini ni masikitiko kuwa watu wabahili wasiokumbuka kufa kwao hawakuikubali bishara hii pia. Na Mungu Alidhihirisha ishara nyingi sana,

lakini hawa wanazikataa zote. Sasa tangazo hili la tarehe 21 Novemba 1898 ni uamuzi wa mwisho. Yapasa sasa kuwa kila mtafutaji mkweli angoje kwa subira. Mungu Hawasaidii waongo, makidhabu na madajjali. Imeandikwa wazi kabisa ndani ya Kurani Tukufu kuwa ni ahadi ya Mwenyezi Mungu kwamba Yeye Huwashindisha waaminio na mitume. Sasa jambo hili liko mbinguni, kupiga kelele ardhini hakusaidii kitu. Makundi yote mawili yako mbele yake na itadhihirika hivi karibuni kuwa nusura na msaada wake unamwendea nani.

وآخر دعوانا أن الحمدلله رب العالمين[7]

والسّلام علٰى من اتبع الهُدىٰ[8]

Mtangazaji
Mnyenyekevu
Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian
30 Novemba 1898

[7] Na mwisho wa maombi yetu ni kuwa sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu. Mwenezi

[8] Na amani iwe kwa waliofuata mwongozo. Mwenezi

## Barua ya Bwana Maulawii Abdullah, Mkazi wa Kashmir

inachapishwa katika tangazo hili kuwanufaisha watu wote, pamoja na ramani ya kaburi la Hadhrat Isa a.s.

Kutoka kwangu Abdullah kwenda kwa mheshimiwa Hadhrat Masihi Mau'udi,

Assalamu alaikum wa rahmatullahi wa barakatuhu.

Mtukufu Hadhrat! Sawa na maagizo yako, mimi baada ya kufika mahali penyewe hasa mjini Srinagar, yaani kwenye kaburi la mwanamfalme, Yuz Asif, Nabii wa Mungu a.s., nikafanya utafiti kwa bidii kadiri ilivyowezekana. Na nikawahoji wazee wenye umri mkubwa, na pia kwa kila jiha nikawauliza-uliza waangalizi wa kaburi na watu waishio katika eneo hilo.

Mheshimiwa, katika kuchunguza nikapata kujua kuwa kaburi hili kwa kweli ni la Mheshimiwa Yuz Asaf a.s. Nabii wa Mwenyezi Mungu. Na kaburi hili lipo katika mtaa wa Waislamu, hakuna Baniani yeyote anayeishi pale, wala hakuna eneo lolote la kuzikia Mabaniani. Na kwa ushahidi wa watu wenye kuaminika, jambo hili limethibitika kuwa kaburi hili lipo tangu miaka 1900 iliyopita. Na Waislamu huliangalia kwa heshima na taadhima kubwa sana na hulizuru. Na watu kwa jumla wanafikiri kuwa ndani

ya kaburi hili amezikwa nabii mmoja mtukufu aliyekuja Kashmir kutoka nchi nyingine kwa ajili ya kuwapa watu nasaha. Na wanasema kuwa nabii huyu alipita miaka kama mia sita kabla ya Mtume wetu s.a.w. Hii haijaeleweka mpaka sasa kwamba kwa nini alikuja nchini humu.[9] Lakini mambo haya bila shaka

---

[9] Nabii yule aliyepita miaka mia sita kabla ya Mtume wetu s.a.w. ni Hadhrat Isa a.s., si mwingine yeyote. Na kuna uwezekano mkubwa kwa neno Yesu kubadilika na kuwa Yuz Asaf, kwani kama neno Yesu limefanywa kuwa **Jesus** kwa Kiingereza, basi hakuna tofauti kubwa kati ya Yuzasaf na Jesus. Neno hili halihusiani kabisa na lugha ya Kisanskrit; laonekana kabisa ni la Kiebrania. Na kwa nini Hadhrat Isa alikuja katika nchi hii? Sababu yake iko wazi, nayo ni hii kuwa Mayahudi wa nchi ya Shamu wasipokubali mahubiri yake na wakataka kumwua msalabani, basi Mwenyezi Mungu, kwa muafaka wa ahadi Yake na kwa kuipokea dua yake, Akamuokoa Hadhrat Masihi a.s. na kifo cha msalabani. Na kama ilivyoandikwa ndani ya Injili kwamba ilikuwemo moyoni mwa Hadhrat Masihi kuwa awafikishie pia ujumbe wa Mwenyezi Mungu wale Mayahudi ambao wakati wa vurugu za Bukhta Nasar, walikuja katika nchi za India. Basi, ni kwa kutimiza lengo hili, yeye alikuja katika nchi hii.

Daktari mmoja Mfaransa, Bw. Bernier, anaandika katika maelezo ya safari yake kuwa, "Watafiti kadhaa wa Kiingereza wamedhihirisha rai zao kwa nguvu sana kuwa wakazi Waislamu wa Kashmiri, kwa kweli, ni Waisraeli waliokuja nchini humo nyakati za vurugu.

yamekwishathibitika na kwa ushahidi unaofululiza yamefikia daraja ya juu ya yakini kuwa Mtakatifu huyo ambaye Waislamu wa Kashmir wameishampa

---

Nyuso za mstatili, kanzu zao ndefu na baadhi ya desturi zao ndio ushahidi wa jambo hili. Basi, yawezekana sana kuwa huenda Hahdrat Isa a.s. baada ya kukatishwa tamaa na Mayahudi wa Shamu akaja katika nchi hiyo kuhubiri kaumu yake. Injili iliyoandikwa hivi karibuni na mtalii mmoja wa Kirusi niliyoiagiza kutoka London, nayo imeafikiana nami katika rai hii kuwa Hadhrat Isa a.s. lazima alikuja katika nchi hii. Na matukio waliyoandika baadhi ya waandishi kuhusiana na Yuz Asaf yaliyoenezwa tafsiri zake katika nchi za Ulaya pia, mapadri nao wameshangaa sana mno wakiyasoma, maana mafundisho hayo yanafanana sana na mafundisho ya kihulka ya Injili, bali ibara nyingi zaonekana kuwa ni zile zile.
Vivyo hivyo Injili ya Kitibeti inafanana sana na mafundisho ya kihulka ya Injili. Hivyo, thibitisho hizi siyo ambazo mtu aweza kuzikatalia mbali kwa nguvu mara moja kiuadui, bali ndani yake mwanga wa ukweli unaonekana dhahiri shahiri. Kuna viashirio vingi sana hata kwamba vikiangaliwa kwa pamoja vyafikisha kwenye natija kwamba hiki si kisa kisicho na msingi. Jina la Yuz Asaf kushabihiana na majina ya Kiebrania, na jina la Yuz Asaf kupata umashuhuri kuwa nabii — neno ambalo latumika kwa manabii wa Kiisraeli na wa Kiislamu pekee, na kisha neno mwanamfalme kuwa pamoja na jina la nabii huyo na halafu sifa za nabii huyo kulingana kabisa na Hadhrat Masihi a.s., na mafundisho yake kuwa sawa na mafundisho ya Kikhulka ya Injili, na kisha yeye kuzikwa

jina la Yuz Asaf ndiye Nabii na pia ni mwanamfalme. Katika nchi hii hakujulikana kwa lakabu yake yoyote ya Kibaniani kama vile *Raja* au *Autar* au *Rikhii* au *Munii* au *Sidd* na kadhalika. Bali wote wanaafikiana kumwita Nabii. Na neno Nabii latumika baina ya Waislamu na Waisraeli kwa usawa. Na kwa vile ndani ya Islam hakuna Nabii yeyote aliyekuja baada ya Mtume wetu s.a.w., wala asingeweza kuja, ndiyo maana Waislamu wa Kashmir kwa jumla wanasema kwa pamoja kuwa nabii huyu ni wa kabla ya Islam. Naam, mpaka sasa hawajafikia uamuzi huu kwamba kwa kuwa neno Nabii latumika kwa manabii wa mataifa mawili tu, yaani kwa manabii wa Kiislamu na wa Kiisraeli, na ndani ya Islam asingeweza kuja Nabii yeyote baada ya Mtume Mtukufu s.a.w., basi imethibitika kabisa kuwa yule ndiye Nabii Mwisraeli

---

katika mtaa wa Waislamu, na halafu muda wa kaburi lake kutajwa kuwa ni miaka elfu moja mia tisa, na kisha katika zama hizi Injili moja kuvumbuliwa na Mwingereza mmoja, na kutokana na Injili hiyo kuthibitika waziwazi ujaji wa Hadhrat Isa a.s. katika nchi hii — natija ya mambo yote hayo, kwa kuyaangalia kwa pamoja, ndiyo kuwa bila shaka yoyote Hadhrat Isa a.s. lazima alikuja katika nchi hii, naye alifia eneo hili hili. Mbali na hayo, kuna hoja nyingine nyingi tutakazoziandika ndani ya kijitabu kingine, Inshallah. — *Kutoka kwa mtangazaji.*

tu, kwani neno hili haikulitumia lugha nyingine yoyote ya tatu. Pasipo shaka, neno hilo lipo katika lugha mbili pekee nalo lahusikana na mataifa mawili tu,[10] lakini kwa sababu ya Khatme Nubuwwat, taifa la Kiislamu limetoka nje, hivyo likaamulika barabara kwamba nabii huyo ni Nabii wa Kiisraeli. Kisha kwa mfululizo wa ushuhuda wa kihistoria kuthibitika kuwa Nabii huyo alipita miaka mia sita kabla ya Mtume wetu s.a.w., kwaongezea yakini zaidi ile hoja ya kwanza na kuelekeza kwa nguvu mioyo yote yenye busara kwenye jambo hili kuwa Nabii huyu ndiye Hadhrat Masihi a.s., si mwingine yeyote awaye. Kwani, ni huyo ndiye aliyepita miaka mia sita kabla ya Mtume Mtukufu s.a.w. Tena, kwa kuzingatia habari hii ifululizayo kuwa Nabii yule anaitwa pia

[10] Tanbihi: Neno nabii lahusikana na lugha mbili tu, na halikutumika katika lugha nyingine yoyote ya ulimwengu. Yaani, kwanza lipo neno hilo katika Kiebrania, na pili, katika Kiarabu. Mbali na hizo, lugha nyingine za ulimwengu hazina uhusiano wowote na neno hilo. Hivyo basi, neno hilo lililotumika kwa ajili ya Yuz Asaf, latoa ushahidi usiokatalika kuwa mtu huyo ama ni nabii Mwisraeli au ni nabii Mwislamu. Lakini baada ya Khatm-e-Nubuwwat, hakuna nabii mwingine anayeweza kuja ndani ya Islam, hivyo imebainika kuwa mtu huyo ni nabii Mwisraeli. Sasa kuuzingatia muda ulioelezwa kwakatiza maneno kuwa huyo ndiye Hadhrat Isa a.s. na ndiye aliyetajwa kwa jina la Mwanamfalme. Mwandishi.

mwanamfalme, uthibitisho huu unakuwa nuru juu ya nuru, kwani katika muda huo hakuna Nabii yeyote minghairi ya Hadhrat Isa a.s., aliyepata umaarufu wa kuitwa Mwanamfalme. Tena jina la Yuz Asaf linalofanana sana na neno 'Yesu' linayatilia nguvu mambo yote hayo ya yakini. Tena kwa kufika mahali pale penyewe, ikajulikana hoja nyingine. Kama ilivyo dhahiri kutoka katika ramani iliyoambatishwa, kaburi la Nabii huyu lipo kusini na kaskazini, na inaonekana kuwa kichwa kipo upande wa kaskazini na miguu upande wa kusini. Na kuzika hivyo huhusikana na Waislamu na watu wa Kitabu. Na uthibitisho mwingine unaotilia nguvu jambo hili ni kwamba kuna mlima unaojulikana kwa jina mlima Sulaiman karibu na kaburi hili. Jina hili pia linaonyesha kuwa hapa aliwahi kuja Nabii wa Kiisraeli.[11] Ni ujahili wa hali ya juu kabisa kumchukulia Nabii huyu Mwanamfalme kuwa Baniani. Na hili ni kosa ambalo mbele ya shuhuda hizo za wazi kabisa hakuna hata


[11] Siyo lazima Sulaiman kuwa nabii Sulaiman, bali yaonekana kuwa yu mfame fulani wa Kiisraeli ambaye kwa jina lake mlima huo ukapata kujulikana. Huenda amiri yule kaitwa jina Sulaiman. Mpaka sasa Mayahudi wanayo mazoea ya kujichukulia majina ya manabii. Kwa vyovyote, jina hilo pia lahakikisha kuwa kundi la Wayahudi lilipita Kashmir ambalo kwa ajili yake ilimbidi Hadhrat Isa a.s. aje Kashmir. Mwandishi.

haja ya kuleta hoja za kulipinga. Katika lugha ya Kisanskriti neno Nabii halipo asilani, bali neno hili ni makhsus kwa Kiebrania na Kiarabu. Na kuzika maiti siyo desturi ya Mabaniani, bali Mabaniani huchoma moto maiti zao. Hivyo, sura ya kaburi pia inayakinisha kabisa kuwa huyo ni Nabii wa Kiisraeli. Upande wa magharibi wa kaburi kuna tundu. Watu wanasema kuwa harufu nzuri sana ilikuwa ikitokea tunduni humo. Tundu hilo ni pana kiasi na linafika mpaka ndani ya kaburi. Inaaminika kuwa tundu hilo liliwekwa kwa kusudio kubwa maalum. Huenda yamefukiwa mle baadhi ya vitu visaidavyo kumtambulisha aliyezikwa humo. Watu wanasema kuna hazina fulani ndani yake, lakini wazo hili halionekani kuaminika. Naam, kwa vile kuweka tundu kama hilo makaburini siyo desturi katika nchi yoyote ile, hivyo inafikiriwa kuwa ndani ya tundu hili kuna siri kubwa sana. Na tundu hilo kuendelea kuwepo kwa mamia ya miaka ni jambo la kushangaza zaidi. Washia wa mji huo nao wanasema kuwa hili ni kaburi la nabii fulani aliyekuwa amekuja toka nchi nyingine kwa kutalii naye aliitwa kwa lakabu ya Mwanamfalme. Washia walinionyesha pia kitabu kimoja kinachoitwa *"Ainul Hayaat"*. Ndani ya kitabu hicho kwenye ukurasa wa 119, mmeandikwa kisa kirefu kwa kurejezwa kwa Ibni Babwaihe na kitabu lkmaluddini na ltmamun Ni'mat, lakini visa vyote hivyo ni vya kipuuzi na kisicho na maana. Ndani ya

kitabu hicho, la kweli ni hili tu kwamba mwandishi wa kitabu anakubali kuwa Nabii huyu alikuwa mtalii na alikuwa mwanamfalme aliyekuja Kashmir. Na njia ya kufikia kaburi la Nabii huyu mwanamfalme ni hii kuwa ukitokea msikiti wa Ijumaa, uje mtaani Raudha Bal Yamiin, kaburi hilo takatifu litakuwa mbele kidogo. Nyuma ya ukuta wa upande wa kushoto wa kaburi hilo kuna njia, na upande wa kulia kuna msikiti wa zamani. Inaonekana kuwa hapo zamani kwa ajili ya kupata baraka msikiti huo ulijengwa karibu na kaburi hilo, na karibu na msikiti huo kuna nyumba za Waislamu. Hakuna hata alama yoyote hapo ya watu wa dini zingine. Na karibu na kaburi la Nabii huyo wa Mungu, kwenye kona ya kulia jiwe moja limewekwa lenye nakshi ya unyayo wa mtu. Yasemekana unyayo huo ni wa Mtume. Labda huo ni unyayo wa Nabii Mwanamfalme uliobakia kama alama. Yaonekana kuna mambo mawili kuhusu kaburi hilo yanayoelekeza kwenye uhakika wa baadhi ya siri zifichikanazo. Mosi, lile tundu lililopo karibu na kaburi. Pili, ni unyayo huo ulionakshiwa katika jiwe. Iliyobakia ni sura ya kaburi ambayo imeonyeshwa kikamilifu katika ramani iliyoambatanishwa.

Hili ni kaburi la Hadhrat Isa a.s. anayejulikana kwa jina la Yesu, Jesus au Yuz Asaf.

Na sawa na ushuhuda wa wazee wa Kashmiri, kaburi hili lipo mjini  Srinagar, mtaa wa Khanyar tangu takriban miaka elfu moja na mia tisa.



# MWISHO WA KITABU

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu na ukarimu wake, ili kuwadhalilisha wapinzani na kudhihirisha ukweli wa mwandishi huyu, imekwishathibitika kuwa lile kaburi lililopo kwa jina la Yuz Asaf, mjini Srinagar katika mtaa wa Khanyar, kwa hakika, pasipo shaka yoyote, ndilo kaburi la Hadhrat Isa a.s. Marhamu ya Isa inayotolewa ushahidi na vitabu elfu moja bali zaidi vya utabibu ni uthibitisho wa kwanza kuwa mheshimiwa Masihi a.s. alisalimika msalabani, kamwe hakufa juu ya msalaba. Katika maelezo ya marhamu hiyo, matabibu wameandika kwa maneno ya waziwazi kabisa kuwa, "Dawa hii hutengenezwa kwa ajili ya aliyepigwa, aliyeanguka na kwa kila aina ya jeraha, nayo ilitayarishwa kutibu majeraha ya Hadhrat Isa a.s., yaani majeraha yake ya mikononi na miguuni mwake." Kwa kuithibitisha marhamu hii, ninavyo pia vitabu vya utabibu vilivyoandikwa kwa mkono tangu miaka 700 iliyopita. Matabibu hao si Waislamu pekee, bali wapo pia Wakristo, Mayahudi na Mamajusi ambao vitabu vyao vipo mpaka sasa. Ndani ya maktaba ya Mfalme Kaisar wa Roma mlikuwa na *Karabadin* (kitabu cha orodha ya madawa na matumizi yake; *famakapia*) kilichoandikwa kwa lugha ya Kirumi. Na kabla haijapita miaka 200 baada ya tukio la msalaba, vitabu vingi vilikwishaenea duniani. Hivyo, msingi wa swala hili kuwa Hadhrat Masihi

hakufia msalabani, kwanza unatokana na Injili zenyewe kama tulivyokwisha eleza tayari, na kisha marhamu ya Isa ikadhihirisha uthibitisho wake kwa utafiti wa kielimu. Kisha ile Injili, iliyopatikana hivi karibuni huko Tibet, imetoa ushahidi dhahiri kuwa Hadhrat Isa a.s lazima alikuja nchini India. Baadaye, kutokana na vitabu vingine vingi, zikajulikana habari za tukio hilo. Katika kitabu cha *Tarikh Kashmir A'dhamii*, kilichoandikwa miaka mia mbili iliyopita, kwenye ukurasa wake wa 82 imeandikwa kuwa, "Kaburi la pili lililopo karibu na kaburi la Seyyid Nasiruddin, hilo lafikiriwa kwamba ni kaburi la mtume fulani". Kisha mwanahistoria huyo anaandika kwenye ukurasa ule ule kwamba "Mwanamfalme fulani alikuja Kashmir akitokea nchi nyingine, naye alikuwa na daraja ya juu sana katika utawa, ucha Mungu, mazoezi ya kidini na ibada. Yeye akateuliwa na Mungu kuwa Nabii na akija Kashmir akashughulikia kuwahubiria Wakashmiri, ambaye jina lake ni Yuz Asaf. Na wengi wenye kupokea kashfi, hususan Mulla Inayatullah aliye kiongozi wangu mimi mwandishi, wamesema kuwa baraka za unabii zinadhihiri kutoka ndani ya kaburi hili." Ibara hii ya *Tarikh A'dhamii* ipo katika lugha ya Kiajemi ambayo imetafsiriwa. Na katika fursa ya kuchambua kitabu kiitwacho "Shahzada Yuz Asaf", kilichoandikwa na Bwana Mirza Safdar Ali, daktari

mpasuaji katika jeshi la serikali ya Nidham, limeandika jarida la *Muhammadan Anglo Oriental College* katika toleo la Septemba 1896 na Oktoba 1896 ya kwamba "Ndani ya kisa mashuhuri cha Yuz Asaf kilichokwisha enea katika Asia na Ulaya, mapadri wameghushi kidogo, yaani katika maisha ya Yuz Asaf yanayofanana sana na mafundisho na khulka za Hadhrat Masihi, labda mapadri wenyewe wameyaongeza ibara hizo." Lakini mawazo hayo yanatokana na kutokuwa na ujuzi. Mapadri walipata kujua maisha ya Yuz Asaf wakati ambapo hayo yalikuwa yameisha julikana tayari katika India na Kashmir na yakaandikwa ndani ya vitabu vya zamani vya nchi hii, na vitabu hivyo vipo mpaka sasa. Basi, mapadri wangeipataje fursa ya kufanya mabadiliko? Naam, mawazo ya mapadri kuwa labda wafuasi wa Hadhrat Masih walikuja nchini humo na ibara hizo katika historia ya Yuz Asaf ndizo zao, wazo hilo ni potofu kabisa, bali sisi tumeshathibitisha kuwa Yuz Asaf ni jina la Bwana Yesu ambalo kutokana na mpishano wa matamshi wa lugha, yametokea mabadiliko kiasi fulani. Hata hivi leo pia baadhi ya Wakashmiri wanasema 'Bwana Isa' badala ya kusema 'Yuz Asaf', kama iliyokwishaandikwa.

والسّلام علٰی من اتبع الهُدیٰ[12]

---

[12] Na amani iwe kwa wafuatao mwongozo. Mwenezi

## Rejeo kuhusu ukurasa wa kwanza
## Tangazo
## Tarehe 30 Novemba 1898.
## Dhila ya haraka.

ذلتِ صادق مجو اے بے تمیز
زیں رہے ہرگز نخواہی شد عزیز[13]

Sheikh Muhammad Husain Batalawii aliendelea kusema mara kwa mara kwamba “Kwa kumchunguza mwongo na mkweli, sisi tunataka kufanya mubahala, na mubahala pia ndio suna katika dini ya Islam. Lakini pamoja na haya kuna ombi hili pia kuwa kama ikithibitika kuwa sisi ni waongo, basi adhabu ituteremkie mara moja. Kwa kuijibu mimi nimeeleza kwa kirefu katika tangazo la tarehe 21 Novemba 1898 kuwa adhabu kushuka mara moja ni kinyume kabisa na suna katika mubahala. Ndani ya Hadithi hadi sasa limo neno la لما حال الحول[14] ambamo Mtume wa Mungu s.a.w. anasema kuwa Wakristo wa Najrani wakiogopa wakaacha kufanya mubahala. Na kama wangefanya mubahala na mimi, mwaka mmoja usingepita wangeangamizwa. Basi, kutokana na Hadithi hii

[13] Tafsiri ya ubeti huu wa Kiajemi:
Ee mtovu wa adabu, usitafute kumfedhehesha mkweli,
kwani, kwa njia hii hutapata kuheshimika. Mwenezi
[14] Kabla haujapita mwaka. Mwenezi

sharti alilotamka Mtukufu Mtume wa Mungu s.a.w. kwa kinywa chake kuhusu mubahala ni mpaka mwaka mmoja. Na desturi hii hii ndiyo suna kwa Waislamu mpaka siku ya kiyama ya kwamba kwa mujibu wa neno hilo la Hadithi hiyo, haipasi kupunguza muda wa mwaka mmoja wa mubahala. Bali waja wa Allah na wenye maarifa ya Mungu walio hoja ya Mungu ardhini wakiwa warithi wa kudumu wa Mtume Mtukufu s.a.w. wamekuwa pia warithi wa muujiza huu ya kwamba kama Mkristo yeyote anayemwamini Hadhrat Isa a.s. kuwa Mungu,[15] au mshirikina mwingine yeyote anayemchukulia mtu fulani kuwa Mungu, akifanya nao mubahala katika jambo hili, basi Mwenyezi Mungu, katika muda huu au katika muda mwingine atakaojua mwenye kufunuliwa kwa njia ya ufunuo atamuonyesha mpinzani wake ishara yoyote ya kimbingu kwa

[15] Inathibitika kutokana na Injili kuwa baraka za kuonyesha ishara katika zama za Hadhrat Isa a.s zilikuwemo ndani ya dini ya Kikristo, bali kuonyesha ishara ilikuwa ni alama ya Mkristo mkweli. Lakini tangu Wakristo walipomfanya mtu kuwa Mungu na kumkadhibisha Mtume Mkweli, kuanzia hapo baraka zote hizo zikawaondoka, na Ukristo ukajifia kama dini zingine. Ndiyo maana, hakuna Mkristo yeyote anayeweza kukabiliana nasi katika kuonyesha ishara za kimbingu. — Mwandishi.

ushahidi wa ushindi wake na ukweli wake. Na hizo ni ishara za kudumu za ukweli wa dini ya Kiislamu ambazo hakuna kaumu yoyote inayoweza kuzikabili. Ilmuradi, muda wa mwaka mmoja ambao ni muda kwa akali kwa bishara za kuonya, wathibitika kutokana na maelezo ya sheria zilizo wazi. Na yule tu atang'ang'ania kutaka adhabu papo hapo ambaye hana kabisa elimu ya Hadithi. Mtu kama huyo anatia doa katika shani ya usheikh. Kwa ajili ya kumfahamisha Bwana Batalawii, nilimwandikia pia kuwa katika mubahala dua mbaya haiombwi na upande mmoja tu, bali huombeana pande zote mbili. Basi, kama kundi moja linaitwa ni la waaminio na Waislamu, na likiliita kundi la pili kuwa kafiri, dajjaal, lisilo na dini, lililolaaniwa na murtadi na linalitoa nje ya Islam, kama alivyo Mian Muhammad Husain wa Batala, sasa ni nani aliyemzuia yeye asiombe adhabu kutokea mara moja? Lakini yule anayefunuliwa wahyi hawezi kufuata matakwa yake. Aletewaye wahyi atafuata tu ufunuo wa Mwenyezi Mungu. Lakini tangazo letu la tarehe 21 Novemba 1898 kuhusu namna ya mubahala lililochapishwa kukabiliana na Sheikh Muhammad Husain na marafiki zake anayewategemea, hiyo ilikuwa ni dua tu ambayo yamaanisha kuwa mwongo apate fedheha kutoka kwa Mwenyezi Mungu; haimaanishi kuwa mwongo auawe au aanguke toka kwenye paa la nyumba. Kwa kuwa

Muhammad Husain, Zatalii na Tibatii wamenitakia fedheha kwa kunizulia uongo, kunilaani na kunitusi, hivyo mimi nimetaka hivi tu kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuwa kama kweli mimi nastahili dhila, ni mwongo, Dajjaal na mlaaniwa kama vile Muhammad Husain alivyoyajaza majarida yake matusi ya aina hii na kuumiza moyo wangu mara kwa mara, basi nidhalilishwe zaidi, na Sheikh Muhammad Husain apate heshima kutoka kwa Mwenyezi Mungu na apate madaraja makubwa. Lakini, kama mimi si mwongo, Dajjaal na mlaaniwa, basi namwomba Mungu aliye mmoja kwamba wanidhalishao hawa, Muhammad Husain na Zatalii na Tibatii, wapate dhila kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Ilmuradi, ninamtaka Mwenyezi Mungu Amdhalilishe mdhalimu na mwongo, awaye yeyote miongoni mwetu sisi wawili, na ninasema amina kwa hiyo. Mimi nimepata ufunuo huu kuwa miongoni mwa makundi haya mawili, kundi lile ambalo machoni mwa Mwenyezi Mungu linadhulumu na linaongopa Mwenyezi Mungu Atalidhalilisha, na habari hii itatimia hadi 15 Januari 1900. Mwenyezi Mungu Anajua vizuri kuwa mbele ya macho yake ni nani aliye mdhalimu na mwongo. Kama katika kipindi hiki, dhila yangu ikidhihirika, bila shaka kuwa kwangu mwongo, mdhalimu na dajjaal kutathibitika, na kwa njia hii ugomvi wa kila siku wa watu utakwisha. Na

kama Sheikh Muhammad Husain, Jaafar Zatalii na Tibatii wakiangukiwa na dhila kutoka mbinguni, basi hii itakuwa ni dalili madhubuti kabisa kuwa wamenidhulumu kwa kunitusi, kuniita dajjaal, mlaaniwa na mwongo. Lakini Sheikh Muhammad Husain, kwa kuukosoa ufunuo wangu wa Kiarabu uliomo ndani ya tangazo la tarehe 21 Novemba 1898 — yaani sentensi hii: اَتَعْجَبُ لِاَمْرِیْ amejifungulia mwenyewe mlango wa dhila, kana kwamba kwa mikono yake mwenyewe amejitimizia utashi wa kupata dhila papo hapo; bali dhila ya mara moja ilitakiwa kutimia kuanzia tarehe 15 Desemba 1898, lakini yeye kabla ya hapo ameshapata fedheha iaibishayo ambayo si ya mara moja bali yapaswa kuitwa fedheha iliyotangulia kabla ya wakati uliowekwa. Nayo ni hii kuwa safari moja Sheikh huyo kwa kuliona tangazo langu hili akaukinza ufunuo huo mbele ya Sheikh Ghulam Mustafaa aliye mwenyeji wa mji huu, kwamba kuna kosa la kisintaksi katika sentensi hii اَتَعْجَبُ لِاَمْرِیْ na maneno ya Mungu hayawezi kuwa na kosa; hiyo ingetakiwa kuwa اَتَعْجَبُ مِنْ اَمْرِیْ. Huu ndio ukinzani uliomfanya Sheikh huyo afedheheke papo kwa papo, maana tumeishathibitisha kutokana na mashairi_ya washairi maarufu wa Kiarabu, bali ya washairi mabingwa wa zama za kabla ya Uislamu, kwamba hata *laam* pia huwa ni kihusishi cha neno *ajab*. Sasa ni wazi kabisa kuwa Sheikh huyo kwa

kuleta ukinzani usiotakikana ulio dalili ya ukosefu wake wa ujuzi, na ujinga wake wa hali ya juu kabisa amejivunjia mwenyewe heshima yake mbele ya wataalamu, na amethibitisha mbele ya adui na rafiki kuwa yu Sheikh wa jina tu, hana ujuzi wa elimu ya Kiarabu. Na hakuna fedheha kubwa kuliko hii kwa mtu anayeitwa Sheikh kwamba kwa kweli hana sifa za usheikh. Ni masikitiko kuwa mtu huyo mpaka sasa hana habari kuwa kihusishi cha kitenzi hicho –yaani *ajab* –pengine hutumika kwa neno *min* na pengine hutumika *laam*. Mtoto aliyesoma mpaka *Hidayatunnahwi,* yeye pia anajua kwamba wataalamu wa kisintaksi wametaja *laam* pia kuwa kihusishi kama walivyoitaja *min*. Basi, kwa ushahidi wa kihusishi hiki beti walizoandika, mmojawapo ni huu pia:

عجبت لمولود ليس له اب      ومن ذی ولد ليس له ابوان

Mshairi ametumia ndani ya ubeti huu vihusishi vyote viwili, *laam* na pia *min*. Na katika *Diwani ya Hamasa* iliyomo ndani ya silabasi ya vyuo vya serikali na ambayo ufasaha wake unakubaliwa, mmeandikwa kwenye kurasa zake za 19, 390, 411, 475, na 511 beti tano za Jaafar bin ‘Ulba na ya washairi wengine, ambamo washairi hao maarufu wa Arabuni wametumia *laam* kuwa ni kihusishi cha neno *ajab*, nazo ni hizi:

عجبتُ لمسراها و انّٰى تخلَّصت — الىَّ و باب السجنِ دونى مُغْلق
عجبت لسعى الدهر بينى و بينها — فلمّا انقضى ما بيننا سكن الدهر
عجبتُ لبُرئى منك يا عزّ بعد ما — عمرت زمانا منكِ غير صحيح
عجبت لعبدان هجونى سفاهة — ان اصبحوا من شأنهم و تقيّلوا
عجباً لاحمد والعجائب جُمّة — انّٰى يلوم على الزمان تبذّلى

Na zaidi ya hayo ni kwamba katika Hadithi iliyomo katika Mishkaat, kitaabul Iman, uk. 3, kuhusiana na maana ya Islam iliyosimuliwa kutoka kwa Mtume Mtukufu s.a.w. — ambayo Hadithi hiyo imekubaliwa na Bukhari na Muslim — humo neno *ajab* limetumika kwa kihusishi cha *laam*. Maneno ya Hadithi ni haya: **عجبنالهيسئلهويُصَدِّقُه**

Angalieni hapa kihusishi cha *ajab* hakikuandikwa *min* bali kimeandikwa *laam*. Hakusema *ajibnaa minhu* bali amesema *ajibnaa lahu*. Sasa bwana Batalawii aseme kuwa je, mbele ya wataalamu hiyo ndiyo dhila ya mwenye kujiita sheikh ama hiyo itaitwa jina jingine? Na hebu utoe fatuwa hii pia kwamba fedheha hii inatakiwa iitwe fedheha ya mara moja au ipewe jina tofauti? Sheikh mwenye chuki kutokana na jadhba ya chuki yake, akaifanya hali yake kuafikiana na ubeti huu:

مرا خواندی و خود بدام آمدی
نظر پختہ ترکن کہ خام آمدی[16]

Yapasa kuangalia kuwa katika kunitafutia dhila yangu, ukadhihirisha dhila yako namna gani. Mtu asiyeijua Hadithi ya kwanza ya Mishkaat na Hadithi iliyo msingi kwa kuutambua Uislamu, hajui hata maneno yake, wala hana habari kabisa ya jambo ambalo limetajwa kwa uwazi ndani ya Bukhari na Muslim hadi sasa ambapo amekuwa mwenye ndevu za mvi. Je mtu mwadilifu anaweza kumwita mtu kama huyo kuwa Sheikh? Basi, mtu ambaye hali ya elimu yake ya Kiarabu ndiyo hii na uhakika wa ujuzi wake wa Hadithi ndio huu kuwa hajui hata maneno ya Hadithi ya kwanza ya Mishkati, bila shaka hali yake ni ya kuhurumiwa, na feheha yake ni nyingi zaidi ya kushinda juhudi za kumsitiri. Na fedheha yake hii bila shaka ni ya papo kwa papo iliyodhihirika ikiwa ishara sawa na ombi lake. Yeye aliomba kwa kinywa chake dhila ya papo kwa papo na Mungu Akaionyesha dhila mara moja.

Nimeshaandika kuwa ufunuo huo hauhusiani na mtu kufa au kuvunjika mguu, huo ndio kwa kudhihirisha dhila ya mwongo. Hivyo, kabla haijadhihirika alama nyingine kubwa zaidi ya Mwenyezi Mungu,

[16] Wewe uliniita (ili kunitega), nawe mwenyewe umetegeka. Imarisha mtazamo wako sana, kwani bado u mbichi. Mwenezi

kudhihirisha dhila, dhila hii pia kwa ajili ya mwongo ni kiboko alichopigwa kwa mkono wa Mwenyezi Mungu. Na katika ufunuo اَتَعْجَبُ لِاَمْرِیْ kuna nukta hii iliyofichikana kwamba ufunuo huu ulikuwa ni bishara iliyofichika kwa ajili ya Muhammad Husain ambamo ilidokezwa kwamba Muhammad Husain ataipinga sentensi hii ya اَتَعْجَبُ لِاَمْرِیْ. Na hiyo yamaanisha kuwa, "Ewe Muhammad Husain, je, unastaajabia neno *liamri,* na unautolea makosa ufunuo wangu huu na unasema kihusishi chake ni *min*. Tazama, mimi nitakuthibitshia kuwa mimi niko pamoja na wanipendao, na nitadhihirisha dhila yako". Basi dhila hiyo ndiyo imedhihirika. Na siyo hiyo tu, kwa sababu Muhammad Husain na marafiki zake, wataimeza fedheha hii kama halua ama kuiynwa kama mtoto kumnyonya mama, hivyo, fedheha iliyoandaliwa mbinguni kwa ajili ya mwongo na mdhalimu ni kubwa zaidi kuliko hii. Mungu Amenifunulia ufunuo kuwa [17]جزاءسیئةبمثلها

Hivyo, kama nimedhalilishwa bila haki, basi mimi natarajia ishara inayohusiana na kumdhalilisha mwongo, mdhalim, mzushi na Dajaal. Na kama mimi ndivyo hivyo, basi nitadhalilika, waila miongoni mwa makundi haya mawili litakalokuwa limedhulumu na

[17] Malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa nao. Mwenezi

kuongopa, basi hilo litaonja ladha ya dhila ile. Zaidi ya kuaibika kielimu, Muhammad Husain na kundi lake wamepata fedheha nyingine pia ya mara moja, nayo ni kwamba kutokana na matukio sahihi na yenye yakini imethibitika kuwa Hadhrat Isa a.s. hakufa msalabani wala hakupaa mbinguni, bali baada ya kuepuka utashi wa Mayahudi wa kumuua alikuja nchini India na hatimaye akafia Srinagar, Kashmir, akiwa na umri wa miaka mia moja na ishirini. Hivyo basi, kwa Muhammad Husain na wengineo huu msiba ni mkubwa na fedheha kubwa. — Mwandishi.